# KITINI CHA URATIBU WA UTAMBULISHO NA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI NCHINI TANZANIA

**JULAI 2025**

## YALIYOMO


**SHUKRANI** .......... **4**

**VIFUPISHO** .......... **5**

**SEHEMU YA KWANZA** .......... **6**

**UTANGULIZI** .......... **6**

**1.0 Utangulizi wa Jumla** .......... **6**

**1.1 Kuhusu KITINI hiki** .......... **6**

**1.2 Malengo ya KITINI Hiki** .......... **7**

**1.2.1 Malengo Mahususi ya KITINI Hiki** .......... **8**

**1.3 Walengwa wa KITINI Hiki** .......... **8**

**1.4 Mchakato wa Kuandika KITINI Hiki** .......... **8**

**SEHEMU YA PILI** .......... **9**

**MFUMO WA KISHERIA** .......... **9**

**2.0 Mfumo wa Kisheria wa Uratibu na Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** .......... **9**

**2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977** .......... **9**

**2.2 Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001** .......... **9**

**2.3 Sheria** .......... **10**

**2.3.1 Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, [Sura ya 56 Toleo la 2023]** .......... **10**

**2.3.2. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), [Sura ya 287 Toleo la 2023]** .......... **10**

**2.3.3. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), [Sura ya 288 Toleo la 2023]** .......... **10**

**2.3.4 Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97** .......... **11**

**2.4 Kanuni kwa ajili ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** .......... **11**

**2.4.1 Kanuni za Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali [Tangazo la Serikali Na. 427 la Mwaka 2004]** .......... **11**

**2.4.2 Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Marekebisho) [Tangazo la Serikali Na. 609 la Mwaka 2018]** .......... **11**

**2.5 Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa Agosti 2024** .......... **11**

**KIBALI CHA MRADI** .......... **13**

**3.1 Kuhusu Kibali** .......... **13**

**3.2 Viambatanisho wakati wa Kuomba Kibali** .......... **13**

**SEHEMU YA NNE** .......... **14**

**UTAMBULISHO WA MRADI** .......... **14**

**4.1 Mamlaka ya Kutoa Barua ya Utambulisho** .......... **14**

**4.2 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotakiwa kuomba Barua ya Utambulisho na Wakati Gani ........ 14**
**4.3 Vigezo vya Kuzingatia na Viambatanisho Wakati wa Kuomba Barua ya Utambulisho ........ 15**
**4.3.1. Vigezo vya kuzingatia wakati wa kuomba barua ya utambulisho** ........ 15
**4.3.2. Viambatisho vya kuwasilisha wakati wa kuomba barua ya utambulisho** ........ 15
**4.4 Mambo ya Kuzingatia Baada ya Kupata Barua ya Utambulisho ........ 15**
**SEHEMU YA TANO ........ 16**
**MAMLAKA ZA USIMAMIZI ........ 16**
**5.1 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ........ 16**
**5.1.1 Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali** ........ 16
**5.1.2 Wasajili Wasaidizi** ........ 16
**5.2 Ofisi ya Rais-TAMISEMI ........ 16**
**5.2.1 Sekretarieti za Mikoa** ........ 16
**5.2.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa** ........ 17
**5.3 Wizara za Kisekta ........ 17**
**SEHEMU YA SITA ........ 18**
**UFUATILIAJI NA TATHMINI WA MIRADI ........ 18**
**6.1 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ........ 18**
**6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mradi ........ 18**
**6.3. Utatuzi wa Malalamiko** ........ 19
**6.4 Adhabu kwa Kukiuka maelekezo ya barua ya Utambulisho ........ 19**
**SEHEMU YA SABA ........ 20**
**HITIMISHO ........ 20**

## SHUKRANI

Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa taasisi zote na wadau waliochangia kwa njia mbalimbali katika maandalizi na uandishi wa KITINI hiki. Shukrani maalum ziende kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kwa ushirikiano wa karibu na mchango mkubwa katika ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na uandaaji wa maudhui ya KITINI hiki.

Tunatambua pia mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zaidi ya 1,000 yaliyoshiriki katika kutoa maoni yao kupitia majukwaa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 143 yaliyoshiriki kutoa maoni kwa njia ya mtandao. Maoni hayo yamekuwa nyenzo muhimu katika kuibua changamoto halisi na mapendekezo ya kuboresha utaratibu wa utoaji wa barua za utambulisho na utekelezaji wa miradi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Shukrani za dhati pia ziende kwa kamati ndogo ya uchambuzi na uandishi wa KITINI hiki iliyojuimisha wataalam kutoka OR-TAMISEMI, NaCoNGO, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na THRDC. Wataalamu hawa ni Dkt. Methusela Massanja-Mkuu wa Dawati la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali OR-TAMISEMI, Anicetus Mramba - Afisa Dawati la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali OR-TAMISEMI, Tulalemwa Mwenda- Wakili wa Serikali OR-TAMISEMI, Abrahamu Mwasha kutoka ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Adamson Kisimba Katibu Mkuu NaCoNGO, Onesmo Olengurumwa- Mratibu Taifa THRDC pamoja na Wakili Paul Kisabo, Lisa Kagaruki, Evaline Mwambungu kutoka THRDC.

Tunathamini kwa dhati juhudi na ushirikiano wa kila mdau aliyeshiriki moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika kuhakikisha KITINI hiki kinapatikana na kuwa andiko muhimu na lenye msaada kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mamlaka mbalimbali za Serikali katika kuimarisha utaratibu wa kuomba na kutoa barua za utambulisho wa miradi pamoja na kuhamasisha uwazi, uwajibikaji, na usimamizi bora wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini Tanzania.

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **MSM**: | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| **NaCoNGO**: | Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| **OR-TAMISEMI**: | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **THRDC**: | Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania |
| **NK:** | Na kadhalika |

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

### 1.0 Utangulizi wa Jumla

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni taasisi huru zinazosajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa na mchango mkubwa katika jamii kwa kuendesha miradi mikubwa ya kijamii kama vile huduma za afya , elimu , maji, msaada wa kisheria nk. Muundo wa KITINI hiki umegawanyika katika Sehemu kuu saba.

a) Sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi wa jumla kuhusu KITINI hiki, malengo ya KITINI hiki pamoja mchakatao uliotumika kuandaa KITINI hiki;
b) Sehemu ya pili ya KITINI hiki inaelezea mifumo ya kisheria inayoratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na mifumo ya kisheria inayoelekeza na kusimamia utaratibu wa utoaji wa barua za utambulisho kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
c) Sehemu ya Tatu inafafanua vibali vya miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vinavyotolewa na Ofisi ya msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
d) Sehemu ya Nne inaelezea kwa undani kuhusu utoaji wa barua za utambulisho, vigezo, taratibu za kuzingatia wakati wa kuomba na mambo ya kuzingatia baada ya kupata barua za utambulisho;
e) Sehemu ya Tano inazungumzia zaidi mamlaka za usimamizi wa utelekezaji wa miradi;
f) Sehemu ya sita inazungumzia utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini, utatuzi wa malalmiko na adhabu zitakazotolewa kwa wale watakaokiuka masharti ya utekelezaji wa mradi husika; na
g) Sehemu ya saba ya KITINI hiki ni hitimisho.

### 1.1 Kuhusu KITINI hiki

Pamoja na kwamba Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanasajiliwa na kuratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zipo taratibu zingine zinazoelekeza taasisi hizi ziende katika ofisi za OR-TAMISEMI ili kupata barua ya utambulisho na uratibu wa utekelezaji wa miradi yao katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM). Barua za utambulisho zimekuwa zikitolewa na kuratibiwa na OR-TAMISEMI kupitia Dawati la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Utaratibu huu umelenga kuipa nafasi Serikali kutambua miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayokwenda kwa wananchi na kujiridhisha kama miradi hii ipo kwa mujibu wa sheria na tamaduni za nchi.

Utaratibu huu wa utoaji wa barua za utambulisho umekuwa ukilalamikiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hii ni kutokana na utafiti mdogo uliofanywa kuanzia mwaka 2022 hadi 2024 na NaCoNGO kwa kushirikiana na THRDC. Malalamiko hayo ni pamoja na kutofahamika kwa utaratibu wa utoaji wa barua za utambulisho, mchakato wa utoaji barua kuwa na mlolongo au

urasimu unaochelewesha utekelezaji wa miradi na vigezo vya kuzingatia na aina ya miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayopaswa kuombewa utambulisho.

Hivyo, KITINI hiki kimeandaliwa kwa ushirikiano wa taasisi za Serikali yaani OR-TAMISEMI, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, NaCoNGO, na THRDC kwa lengo la kufafanua zaidi malengo na utaratibu wa utoaji wa barua za utambulisho. KITINI hiki kinaendeleza ufafanuzi kwa kina zaidi ambao umekuwa ukitolewa na OR-TAMISEMI kama maelekezo kwa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Barua ambazo zimekwisha tolewa kufafanua utaratibu huu ni pamoja na barua zifuatazo:

a) Barua yenye Kumb. Na. JC 15612541A11A41 ya tarehe 09 Januari 2024;
b) Barua yenye Kumb. Na. JC 15612541A1 ya tarehe 4 Septemba 201;
c) Barua yenye Kumb. Na. JC 1561254101 ya tarehe 04 Julai, 21; na
d) Barua yenye Kumb. Na. 8A.3221343111 ya tarehe 09 Mei, 2023.

Pamoja na maelekezo yaliyotolewa katika barua hizo, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuzingatia taratibu hizo na ufafanuzi wa KITINI hiki wakati wa kutuma maombi, kutoa barua ya utambulisho na wakati wa utekelezaji wa miradi.

Kwa uwepo wa barua hizo za ufafanuzi zinazojibu baadhi ya hoja ni dhahiri kwamba kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo wa kisheria utakaoelezea kwa kina utaratibu, kuainisha masharti na vigezo vya uombaji na utoaji barua za utambulisho. Hivyo KITINI hiki sio mwongozo wa kisheria bali ni ufafanuzi rahisi wa utaratibu, masharti na vigezo kwa lengo la kuwasaidia waombaji na watoaji wa barua hizo pamoja na wasimamizi wa miradi katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalipendekeza kuwepo mwongozo wa kisheria, KITINI cha ufafanuzi na mfumo jumuishi wa kidijitali ili kutatua malalamiko yaliyobainishwa. Hivyo KITINI hiki kinatoa ufafanuzi rahisi kuhusu utaratibu wa uombaji na utoaji wa barua za utambulisho kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. KITINI hiki kinaweza kisiwe kimejitosheleza katika kila hoja iliyohitaji ufafanuzi na pia KITINI hiki sio mbadala wa sheria au mwongozo wowote wa kiserikali.

## 1.2 Malengo ya KITINI Hiki

KITINI hiki kimeandaliwa kwa lengo la kutoa ufafanuzi rahisi na unaoeleweka kuhusu utaratibu wa kuomba na kutoa barua za utambulisho za utekelezaji wa miradi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Lengo kuu ni kuwezesha mashirika haya kuelewa taratibu za kisheria na kiutendaji, kuhakikisha utekelezaji wa miradi unakuwa bora, wa haraka, wenye uwazi na unaozingatia sheria za nchi kwa maendeleo endelevu.

### 1.2.1 Malengo Mahususi ya KITINI Hiki

a) Kutoa elimu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusu mfumo wa kisheria, kibali cha mradi, barua za utambulisho wa miradi, mamlaka za usimamizi na ufuatiliaji na tathmini;

b) Kutoa ufafanuzi kuhusu utofauti wa kibali cha miradi na barua ya utambulisho wa miradi pamoja na hatua za kuchukua iwapo kuna Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakuwa hayajaridhika na maamuzi katika barua ya utambulisho;

c) Kuimarisha ushirikiano kati ya OR-TAMISEMI, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekretarieti za Mikoa, MSM, NaCoNGO na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika hatua zote za utoaji vibali vya miradi, barua za utambulisho, utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi;

d) Kubainisha misingi ya uwajibikaji na ufuatiliaji kwa kufafanua wajibu wa Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika tathmini ya utekelezaji wa miradi; na

e) Kuainisha hatua zitakazochukuliwa endapo masharti ya utekelezaji wa miradi yatakakiukwa.

## 1.3 Walengwa wa KITINI Hiki

Walengwa wa KITINI hiki ni OR-TAMISEMI, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara za Kisekta, Mikoa, MSM, NaCoNGO na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hivyo, KITINI hiki kimewalenga Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (katika ngazi za Kimataifa, Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya).

Hadi tarehe 19 Julai 2025, kuna jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 11,163 yanayofanya kazi Tanzania Bara, yakitekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuchangia juhudi za Serikali kufikia malengo mbalimbali ya maendeleo.

## 1.4 Mchakato wa Kuandika KITINI Hiki

Mchakato wa kuandika KITINI hiki ulitokana na utafiti mdogo uliofanywa na THRDC kwa kushirikiana NaCoNGO ulioanza mwaka 2022.

Mnamo mwaka 2022 hadi 2024 THRDC na NaCoNGO walikusanya maoni kupitia njia mbalimbali ikiwemo dodoso maalum, majukwaa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kitaifa, Mikoa na Wilaya. Zaidi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,000 yalifikiwa katika majukwaa hayo, na jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 143 yalitoa maoni kwa njia ya mtandao.

# SEHEMU YA PILI
# MFUMO WA KISHERIA

## 2.0 Mfumo wa Kisheria wa Uratibu na Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Sehemu hii inafafanua mfumo wa Kisheria unaoratibu na kusimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara. Sheria hizo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97, Kanuni za Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali [Tangazo la Serikali Na. 427 la Mwaka 2004], Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Marekebisho) [Tangazo la Serikali Na. 609 la Mwaka 2018], na Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa Agosti 2024.

### 2.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Katiba ndiyo sheria mama inayotambua haki ya wananchi ya kuanzisha na kushiriki katika shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ibara ya 20(1) ya Katiba imeainisha kuwa: *"Kila mtu anao uhuru wa kuanzisha na kushiriki katika mashirika kwa madhumuni ya kulinda au kuendeleza maslahi yake."*

Pia, Ibara ya 18 imeainisha kuwa kila mtanzania ana haki ya kutoa maoni, kupewa taarifa ya mambo ya msingi, ikiwa ndio ni msingi muhimu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hasa yanayojihusisha na utetezi na uhamasishaji na kuweka msingi wa kikatiba kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Pia inasisitiza ushirikishwaji na ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo yao.

Aidha, Ibara ya 145 imeainisha uanzishaji wa vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mkoa, Wilaya, Mji na Kijiji.

Na Ibara ya 146 imeainisha wajibu wake ikiwa ni pamoja na kushirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na ulinzi wa wananchi.

### 2.2 Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001

Sera hii ilitolewa mwaka 2001 kwa lengo la kuweka mwongozo wa kisera kuhusu usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Sera hii inatambua mchango mkubwa wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya taifa, inasisitiza ushirikiano baina ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, inalenga kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kufanya kazi kwa uhuru, lakini kwa kuzingatia uwajibikaji na inatilia mkazo umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na miundo madhubuti ya ndani, utawala bora, na mfumo mzuri wa kifedha. Sera hii ndiyo iliyopelekea kuandaliwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2002.

### 2.3 Sheria

#### 2.3.1 Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, [Sura ya 56 Toleo la 2023]

Sheria hii ndiyo inayosimamia uanzishwaji, usajili, uendeshaji na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara. Sheria hii inatoa tafsiri ya Shirika Lisilo la Kiserikali kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya marekebisho Na. 3 ya mwaka 2019. Sheria imeainisha vyombo vya kisheria vya usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwemo Ofisi ya Msajili, Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Pia inaainisha taratibu na ngazi za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Kimataifa, kitaifa, kimkoa na kiwilaya na kuainisha vyombo vya utatuzi wa migogoro ambavyo ni Ofisi ya Msajili, Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Waziri mwenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Aidha, Kifungu cha 32 kimeainisha takwa la mashirika yote yaliyosajiliwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa nyaraka zao za usajili.

Sheria inampa mamlaka Msajili kuteua Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Mikoa na MSM ambao wanajukumu la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na inampa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni za Usimamizi. Aidha, Sheria imeainisha makosa na adhabu

#### 2.3.2. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), [Sura ya 287 Toleo la 2023]

Kifungu cha 184 kimeainisha wajibu wa Serikali Kuu kwa MSM ikiwa ni pamoja na kuwakasimisha majukumu yake na kuwatambulisha watu wanaokwenda kufanya kazi maeneo yao. Huo ndio msingi wa uwepo wa utaratibu wa kutoa barua ya utambulisho.

Aidha, Kifungu cha 115(1) (b) kimeainisha wajibu wa Halmashauri ya Wilaya kusimamia na kukuza ustawi wa jamii katika maeneo yao ya mamlaka. Hii ikiwa na maana kuwa Halmashauri ya Wilaya ina wajibu wa kutambua, kusimamia na kufuatilia miradi ambayo inatekelezwa na kugusa jamii. Huu ndio msingi wa uwepo wa utaribu usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi za MSM. Kutimiza majukumu haya isitafsiriwe kama kuingilia uhuru wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali bali ni majukumu ya kisheria kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayogusa jamii inatambuliwa, inaratibiwa na ipo kwa mujibu wa sheria za Tanzania na tamaduni.

#### 2.3.3. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), [Sura ya 288 Toleo la 2023]

Kifungu cha 63 kimeainisha wajibu wa Serikali Kuu kwa MSM ikiwa ni pamoja na kuwakasimia majukumu yake na kuwatambulisha watu wanaokwenda kufanya kazi maeneo yao. Huo ndio msingi wa uwepo wa utaratibu wa kutoa barua ya utambulisho wa miradi

Na Kifungu cha 62(1) (b) kinaainisha wajibu wa Halmashauri za Miji kusimamia na kukuza ustawi wa jamii katika maeneo yao ya mamlaka. Hii ikiwa na maana kuwa Halmashauri ya Wilaya ina wajibu wa kutambua, kusimamia na kufuatilia miradi ambayo inatekelezwa na kugusa jamii. Huu ndio msingi wa uwepo wa utaribu usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi za MSM. Kutimiza majukumu haya isitafsiriwe kama kuingilia uhuru wa Mashirika Yasiyo ya

Kiserikali bali ni majukumu ya kisheria kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayogusa jamii inatambuliwa, inaratibiwa na ipo kwa mujibu wa sheria za Tanzania na tamaduni.

#### 2.3.4 Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura ya 97

Kifungu cha 11 kimeainisha majukumu ya Sekretarieti ya Mkoa kuwa ni pamoja na kutekeleza majukumu yoyote ndani ya mkoa ambayo yametolewa na Serikali kwa mujibu wa sheria na sheria nyingine au yanaweza kuelezwa na Waziri kupitia tangazo lililochapishwa katika Gazeti la Serikali. Hii ndio msingi wa Sekretarieti za Mikoa kusimamia utekelezaji wa kila jambo katika mikoa na kuzisimamia na kuzisaidia MSM kutekeleza majukumu yake.

### 2.4 Kanuni kwa ajili ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

#### 2.4.1 Kanuni za Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali [Tangazo la Serikali Na. 427 la Mwaka 2004]

Kanuni hizi zimeainisha utaratibu wa usajili wa mashirika, mabadiliko ya majina, anwani za ofisi, na uwasilishaji wa taarifa ambazo ni pamoja na mapato, matumizi, shughuli zilizotekelezwa, na mipango ya baadae ya shirika husika kwa Msajili. Pia zinaainisha utaratibu wa kushughulikia mabadiliko ya uongozi wa mashirika. Vilevile, zinaelekeza namna mashirika yanavyopaswa kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mujibu wa malengo yao yaliyoainishwa katika katiba ya usajili.

#### 2.4.2 Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Marekebisho) [Tangazo la Serikali Na. 609 la Mwaka 2018]

Kanuni hizi zimeweka masharti ya kiutawala na kuanzisha makosa ya kijinai kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi Tanzania Bara.
**Kanuni ya 12**, inayataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa taarifa za kina kuhusu vyanzo vya fedha, madhumuni, matumizi, na shughuli zilizopangwa kufanyika kwa Mamlaka mbalimbali ndani ya siku kumi na nne baada ya kukusanya fedha.
**Kanuni ya 13** inataka kila Shirika Lisilo la Kiserikali linalopokea kiasi cha fedha kinachozidi shilingi milioni ishirini (20,000,000) kuchapisha taarifa za mapato hayo mara mbili kwa mwaka katika magazeti yanayosambazwa sana au vyombo vingine vya habari vinavyofikiwa na wananchi kwa urahisi. Pia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuwasilisha nakala za mikataba au makubaliano yoyote na wafadhili katika Wizara ya Fedha na Ofisi ya Msajili ndani ya siku kumi (10) tangu kusainiwa kwa makubaliano hayo ili yaidhinishwe.
**Kanuni ya 15(2)**, inaanzisha kosa la jinai endapo kuna ukiukwaji wa masharti ya kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

### 2.5 Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa Agosti 2024

Mwongozo huu uliandaliwa kwa ajili ya kuweka misingi imara ya ushirikiano wa pamoja na kuainisha majukumu kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, MSM, Sekta Binafsi na

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kusimamia na kuratibu utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

Lengo kuu la Mwongozo huu ni kuondoa muingiliano na mgongano wa kiutendaji na kuimarisha uratibu wa pamoja wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kati ya Wizara yenye dhamana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, MSM, Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

## SEHEMU YA TATU

## KIBALI CHA MRADI

### 3.1 Kuhusu Kibali

Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 ilipelekea kutungwa kwa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56, na Sheria Na.11 ya mwaka 2005 na Sheria Na.3 ya mwaka 2019. Kanuni mbalimbali zimetungwa ikiwa ni pamoja na Kanuni Na.609 ya mwaka 2018 iliyotoa ufafanuzi wa utekelezaji wa Sheria hiyo kuhusu uwazi na uwajibikaji wa fedha.

Pamoja na mambo mengine, Kanuni ya 13(a), (b) na (c) ya Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 zimeweka utaratibu madhubuti wa uzingatiaji wa taratibu za kifedha za mapato, matumizi na manunuzi kwenye Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Kanuni hizo zimeainisha mambo yafuatayo;

i. Utaratibu kuwasilisha mikataba mbalimbali ya fedha za wafadhili zinazozidi Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000/=) kwa Msajili ili atoe kibali cha miradi husika kwenye afua zilizoelezwa kwenye mkataba ikilinganishwa na malengo ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali husika; na
ii. Kudhibiti uingiaji wa mikataba ya ufadhili inayokinzana na Sheria za Tanzania na tamaduni.

### 3.2 Viambatanisho wakati wa Kuomba Kibali

Wakati wa kuomba kibali cha utekelezaji wa miradi viambatanisho vifuatavyo huitajika;

i. Mkataba wa ufadhili (funding contract);
ii. Mpango Mkakati (strategic plan);
iii. Mpango Kazi (Work plan);
iv. Fomu ya Mkataba wa maombi ya mradi (Project Application form Contract);
v. Uthibitisho wa kuukubaliwa kwa mradi kutoka Wizara yenye dhamana (Initial Approval of the Project from Relevant Ministry); na
vi. Uthibitisho wa kuweka fedha (Proof of Deposit).

Ifahamike kwamba, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaruhusiwa kuanza kazi baada ya kusajiliwa na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Usajili ambao unaodumu kwa muda wa miaka 10. Aidha, utaratibu wa kupeleka mikataba ya fedha kwa msajili na kupewa kibali cha miradi umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha serikali inakuwa na kumbukumbu ya fedha zote zinazoingia kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na pia kujiridhisha na vyanzo vya fedha pamoja na miradi inayokwenda kutekelezwa.

## SEHEMU YA NNE
## UTAMBULISHO WA MRADI

### 4.0 Barua za Utambulisho wa Mradi

Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kutekeleza majukumu yake hasa katika eneo la ustawi wa jamii inajukumu la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzitambua, kuzitambulisha na kuzisimamia kabla na baada ya usajili, baada ya kupata vibali vya miradi na wakati wa utekelezaji wa miradi. Hivyo kabla ya usajiliwa inajukumu la kuzitambulisha kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na baada ya kupataa kibali cha mradi inatakiwa kuzipatia barua ya utambulisho ili kuanza utekelezaji wa miradi katika eneo la Mkoa na MSM. Aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanawajibu wa kuomba barua ya utambulisho katika OR-TAMISEMI. Hivyo ni vema kutofautisha kati ya vibali vya miradi vinavyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na barua ya utambulisha wa miradi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inayotolewa na OR-TAMISEMI.

### 4.1 Mamlaka ya Kutoa Barua ya Utambulisho

Ofisi ya Rais-TAMISEMI ndio mamlaka yenye wajibu wa kutoa barua ya utambulisho kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa na lengo la kutambulisha, kusimamia na kufanya ufuatiliji wa utekelezaji wa wa miradi. Kikatiba na Kisheria OR-TAMISEMI ndio inasimamia shughuli zote za kijamii na kimaendeleo katika ngazi za Mikoa na MSM. Hivyo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatakiwa kuomba Barua ya Utambulisho kutoka OR-TAMISEMI kabla ya kwenda kutekeleza miradi katika ngazi za Mikoa na MSM.

### 4.2 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotakiwa kuomba Barua ya Utambulisho na Wakati Gani

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyopata kibali cha mradi au inayotaka kutekeleza mradi katika eneo la Mkoa au MSM inawajibu wa kuomba barua ya utambulisho kutoka OR-TAMISEMI kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi katika eneo husika.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye mradi wenye thamani ya zaidi ya milioni ishirini au chini ya milioni ishirini yote yanahitaji kupata barua ya utambulisho kutoka OR-TAMISEMI kama miradi yao inagusa jamii na watumishi wa umma. Pamoja na kwamba vibali vya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutolewa zaidi kwa mashirika yenye miradi ya thamani ya million ishirini na kuendelea , kwa upande wa OR-TAMISEMI barua ya utambulisho ni kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye miradi kwa jamii na watumishi wa umma bila kujali gharama za utekelezaji wa mradi. Hoja ya Msingi hapa ni utambulisho wa miradi ili viongozi wa maeneo hayo waweze kusimamia, kufuatilia na kutoa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa jamii.

### 4.3 Vigezo vya Kuzingatia na Viambatanisho Wakati wa Kuomba Barua ya Utambulisho

Wakati wa kuwasilisha maombi ya barua ya utambulisho, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatakiwa kuzingatia vigezo na kuwasilisha viambatisho vifuatavyo:

#### 4.3.1. Vigezo vya kuzingatia wakati wa kuomba barua ya utambulisho

a) Wasilisha barua yenye anuani kamili na hai ya Shirika Lisilo la Kiserikali ikiainisha anuani ya posta, barua pepe ya shirika, na namba ya simu ya shirika au Kiongozi mwenye Mamlaka; na

b) Wasilisha mpangokazi wa utekelezaji wa mradi ulioainisha vitu vifuatavyo:

   i. jina la mradi na eneo la utekelezaji wa mradi ukiainisha Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa;

   ii. ainisha chanzo cha mapato, gharama za mradi;

   iii. taja wanufaika wa mradi husika;

   iv. taja muda wa utekelezaji wa mradi ukianisha tarehe ya kuanza na kumaliza utekelezaji wa mradi; na

   v. taja gharama za mradi

#### 4.3.2. Viambatisho vya kuwasilisha wakati wa kuomba barua ya utambulisho

a) Nakala ya cheti cha usajili na risiti ya malipo ya ada ya mwaka ya Shirika Lisilo la Kiserikali husika (hii ni kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yenye miradi ya thamani chini ya million ishirini);

b) Nakala ya kibali cha mradi kutoka ofisi ya msajili (hii ni kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo yana miradi yenye thamani zaidi ya millioni ishirini);

c) Nakala ya mkataba wa ufadhili wa miradi yenye thamani chini ya Shiliingi milioni ishirini au mingine; na

d) Mpangokazi wa utekelezaji wa mradi.

### 4.4 Mambo ya Kuzingatia Baada ya Kupata Barua ya Utambulisho

a) kuwasili/kufika katika mamlaka husika uliyotambulishwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi;

b) kushirikiana na mamlaka husika uliyotambulishwa katika utekelezaji wa mradi;

c) kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Nchi;

d) kuzingatia mila, desturi na tamaduni za nchi; na

e) kuzingatia maelekezo ya barua ya utambulisho.

## SEHEMU YA TANO
## MAMLAKA ZA USIMAMIZI

**5.0 Mamlaka za Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Ili kuleta usimamizi mzuri wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa usajili, usimamizi, ufuatiliaji na tathimini. Katika kutekeleza jukumu hiki la usimamizi na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, zipo mamlaka mbalimbali za usimamizi kama ifuatavyo:

**5.1 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

Wizara hii imepewa mamlaka ya kusajili  na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotaka kufanya kazi nchini, kutoa kibali cha mradi, kufuatilia utendaji wao kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na wadau wengine.

**5.1.1 Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maaalum anajukumu la kusajili, kutoa kibali cha mradi, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini.

**5.1.2 Wasajili Wasaidizi**

Wasajili wasaidizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wanateuliwa na Mjasili na  wanajukumu la kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Wasajili wasaidizi hufanya kazi wakiwa katika Sekretarieti za Mikoa na MSM.

### 5.2 Ofisi ya Rais-TAMISEMI

Ofisi ya Rais-TAMISEMI ina wajibu wa kusimamia na kuhakikisha maendeleo na ustawi wa Jamii, Kwa kuwa OR-TAMISEMI ndiyo inayozisimamia Sekretariati za Mikoa na MSM, hivyo inajukumu la kutoa barua ya utambulisho wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa maeneo hayo. Barua ya utambulisho itatolewa baada ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kusajiliwa, na kupata vibali vya miradi. Pamoja na wajibu huo OR-TAMISEMI itafuatilia utendaji wa kazi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Mikoa na MSM.

### 5.2.1 Sekretarieti za Mikoa

Sekretarieti za Mikoa ni moja ya ngazi ya utendaji katika OR-TAMISEMI ambayo husimamia na kutekeleza majukumu yote ya Mkoa na kusimamia utendaji wa MSM. Ili kuwa na utekelezaji mzuri wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekretarieti za Mikoa zina Seksheni ya Mipango na Uratibu ambayo inawajibika kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya Mkoa kupitia Msajili Msaidizi ambae ameteuliwa na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza jukumu la kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Mikoa na MSM.

### 5.2.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) zinajukumu la kusimamia na kuhakikisha uwepo wa maendeleo na ustawi wa jamii katika eneo lake la Mamlaka. Divisheni ya Maendeleo ya Jamii katika MSM kupitia Msajili Msaidizi ndio yenye jukumu la kusimamia, kufuatilia na kutathimini shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

## 5.3 Wizara za Kisekta

Kuna Wizara za Kisekta ambazo zinajukumu la kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na majukumu ya Kisekta nchini (mfano ni Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Mambo ya Ndani). Katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wameanzisha madawati ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuleta unafuu wa utekelezaji wa majukumu yao.

## SEHEMU YA SITA
## UFUATILIAJI NA TATHMINI WA MIRADI

### 6.0 Ufuatiliaji na Tathmini

Katika utekelezaji wa miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ufuatiliaji na tathmini ni sehemu muhimu sana ili kufikia malengo. Hatua hii inasaidia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kubaini mapungufu kwa wakati kabla ya kufikia mwisho wa mradi. Inasaidia kufanya maamuzi ya mabadiliko katika utekelezaji wa mradi kama kutakuwa na haja hiyo ili mradi ufikie malengo yake.

### 6.1 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi

Ufuatiliaji hupaswa kufanyika sambamba na utekelezaji wa mradi. Mashirika mengi yana taratibu zake za kufanya ufuatiliaji pengine kila siku, kila wiki au kila mwezi kutegemea na mpango wa shirika.

Hakuna mpango rasmi wa pamoja kati ya Mashirika na OR-TAMISEMI. Kile kinachoweza kuonekena kama ufuatiliaji wa miradi ya wadau ni pale wadau hao wanapolazimika kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi yao kila robo mwaka. Wasajili wasaidizi katika ngazi ya Halmashauri wanajukumu kubwa la kuona kuwa taarifa zinazowasilishwa ni halisi na za kweli. Ufuatiliaji unajikita zaidi katika kujua kama waliopewa kibali cha miradi na barua ya utambulisho wamefika eneo husika na kama wanatekeleza miradi kwa misingi ile ile ambayo vibali na barua hizo zilitolewa. Pia ufuatiliaji huu unalenga kuangalia kama sheria za nchi na masharti ya msingi yanazingatiwa wakati wa utekelezaji wa miradi kwa kuwa kumewepo pia na mazingira ya mashirika kutekeleza miradi tofauti na kibali na barua za miradi.

OR-TAMISEMI ilishazielekeza MSM kutenga fedha kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza tija na umiliki (ownership) wa miradi hiyo. Ni vyema ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi katika ngazi za taifa, mikoa na MSM kufanyika kwa pamoja na kuboresha mawasaliano kati ya mamlaka zote za usimamizi.

### 6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mradi

Hiki ni zoezi muhimu katika kubaini malengo ya mradi yamefikiwa kwa kiasi gani. Tathmini ya miradi hufanywa na Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na matokeo yake husambazwa kwa wadau wengine.

OR-TAMISEMI imeelekeza Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yote kuhakikisha yanatenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza jukumu la kufanya tathmini. Kutokana na tathmini, tunajifunza mambo mengi ambayo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mengine yanaweza kujifunza na kuchukua tahadhari.

### 6.3. Utatuzi wa Malalamiko

Katika utekelezaji wa wajibu wa kuomba na kupata barua ya utambulisho malalamiko yatatatuliwa kwa njia ya maridhiano kati ya pande zote mbili yaani Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Idara ya Uratibu na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kama hawatafikia muafaka, malalamiko hayo yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI ambae atatoa uamuzi na na kama ataona malalamiko hayo yamefikia hatua ya mgogoro atashauri kufuata taratibu za utatuzi wa migogoro zilizowekwa na sheria au kanuni husika.

### 6.4 Adhabu kwa Kukiuka maelekezo ya barua ya Utambulisho

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakayo kiuka maelekezo ya barua za utambulisho yatafutiwa barua ya utambulisho na kusitishwa kwa utekelezaji wa miradi katika maeneo husika na kama kuna makosa ya kisheria yaliyofanyika basi utaratibu ulioainishwa katika sheria husika utatumika.

## SEHEMU YA SABA
## HITIMISHO

### 6.1 Hitimisho

Kwa ujumla, kupitia KITINI hiki, inatarajiwa kuwa uataratibu wa kuomba na kupewa barua za utambulisho pamoja na utekelezaji wa miradi utakuwa umeelezewa na kueleweka kirahisi. Vilevile kupitia KITINI hiki ushirikiano kati ya serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali utaimarika zaidi, na kuimarisha nafasi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuchangia maendeleo ya kijamii nchini. Kupitia KITINI hiki tunategemea changamoto zilizokuwa zinaibuliwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zitakuwa zimetatuliwa kwa sehemu kubwa.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa na mchango mkubwa katika kuchangia jitihada za maendeleo hapa nchini na wamekuwa wakifanya kazi katika afua mbalimbali kama huduma za afya, maji , elimu , msaada wa kisheria , haki za makundi maalum, haki za binadamu, mabadiliko ya tabia nchi, kilimo , uchumi na utawala bora.  Kutokana umuhimu wa sekta hii ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ni vema kuweka mazingira wezeshi na yasiyo na vikwazo ili kuwasaidia waweze kuwafikia wananchi kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa. KITINI hiki ni sehemu ya kuhakikisha mchakato wote wa uombaji na utoa barua za utambulisho unafanyika kwa ufanisi na kwa wakati ili kutoa nafasi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwahudumia watanzania.